

Maswali

1. Mbona Mungu alitaka waharibu watu walioabudu sanamu kwa nchi.
2. Taifa gani lilishambulia nchi ya Israeli ?
3. Waliwanyanyaza namna gani ?
4. Mbona Gideoni hakutaka kufanya alichoambiwa na malaika?
5. Ni ishara gani ilikuwa ya kuonyesha Gideoni kwamba Mungu atakuwa naye?
6. Gideoni alitumia Waisraeli wangapi kushinda Wamidiani?
7. Mbona walikuwa wachache?
8. Kila mtu alipewa nini kama silaha
9. Mbona walipiga kelele walipovunja mitungi?
10. Tunajifunza nini kwa habari hii?

Majibu

1. Kwa sababu watu waabuduo sanamu wangewahusisha Waisraeli kuabudu sanamu.
2. Wamidiani
3. Waliharibu mimea.
4. Kwa sababu alihizi uoga na kujifikiria hangeweza
5. Ngozi iliyokuwa na unyevu wakati ardhi ni kavu
6. 300
7. Kwa sababu Mungu alitaka kuonyesha ni yeye aliyeshinda vita.
8. Mwenge ndani ya mtungi na tarumbeta
9. Upanga wa Bwana na wa Gideoni.
10. Kwamba Mungu atatusaidia tukimwamini.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



8 Hadithi ya Gideoni

Marejeo

Waamuzi 6 + 7

Kiini cha somo

Tunapokuwa hatuna uhakika, tumgeukie Mungu atuonyeshe njia, tusitumainie nguvu zetu

Maneno maalum

1. Watu wateule wa Mungu + Mungu alikuwa mfalme.
2. Sanamu + Wamidiani + mimea + vilima.
3. Muamuzi + Gideoni + ngozi ya kondoo
4. 32,000 + tishika + shinda
5. Nyumbani + kunywa +300 + chota
6. Mwenge (tochi) uwakao + tarumbeta + bila silaha.
7. Upanga wa bwana na wa Gideoni.
8. Shinda + bariki + miaka 40.

8.1 Waisraeli ni watu wateule wa Mungu. Hii hadithi ilitendeka wakati walikuwa wakiishi kwa nchi walioahidiwa na Mungu. Hawakukuwa na mfalme wa kuwatawala. Mungu ndiye alikuwa mfalme wa Israeli wa kweli. Mara nyingi hawakukumbuka haya. Walipoasi Mungu aliwaadhibu ili wamkumbuke na wamtegemea yeye.

8.2 Wana wa Israeli walipowasili nchini, Mungu aliwambia waangamize watu wote walioabudu sanamu. Lakini hawakufanya hivi, hata wengine walianza kuabudu hizo sanamu. Kuwaadhibu, Mungu alitumia taifa liitwalo Midiani kuwashambulia. Biblia inasema Wamidiani walikuwa wengi sana hata hawangeweza kusabuliwa. Waliingia kwa nchi ya Israeli na n'gombe zao na wakaharibu mimea. Waisraeli wengi walihama na kwenda kuishi kwa vilima. Baada ya miaka 7 waliamua kuita Mungu awasaidie.


8.3 Mungu aliwapa Waisraeli kiongozi (aliyeitwa waamuzi) atakaye waokoa. Malaika alimtokea mtu aitwae Gideoni na akamwambia kwamba ataokoa Israeli kutoka kwa Wamidiani. Gideoni alishangaa sana. Akasema, "Nitawaokoaje Israeli- mimi ndie mtoto sana kwa familia tena jamii yangu ndio hafifu kwa kabila letu." Malaika alimjibu kwamba Mungu atakuwa naye na atamwambia cha kufanya. Bado Gideoni hakuamini kwa hivyo akauliza Mungu kuwe na ishara ya kumuonyesha kwamba ataokoa Israeli. Aliweka ngozi ya kondoo nje ya nyumba usiku kucha. Akamwambia Mungu, asubuhi kukiwa na umande juu ya ngozi ya kondoo na ardhi imekauka nitajua wewe uko na mimi. Hivyo ilikuwa siku ifwatayo. Gideoni alienda nje asubuhi na kupata umande kwa ngozi ya kondoo na ardhi imekauka.

8.4 Kwa hivyo Gideoni akakusanya watu Israeli ili waende wapigane na Wamidiani. Walikuwa watu 32,000, ingawaje walikuwa wengi lakini Wamidiani walikuwa zaidi, walikuwa 135,000. Waisraeli wakaogopa SANA. Mungu akamwambia Gideoni kwamba jeshi la Israeli ni kubwa zaidi. Alitaka jeshi ndogo, ili maadui wakishindwa Waisraeli wajue ni Mungu amefanya.

8.5 Gideoni aliuliza kama kuna yeyote aliyekuwa muoga na arudi nyumbani. Watu 22,000 walirudi wakabaki 10,000. Lakini Mungu alisema kwamba bado walikuwa wangali wengi sana. Akawapa jaribio ndogo. Akawambia, "Enda kando ya mto na watu wote ili wanywe maji." Watu 300 walichota maji kwa mikono lakini wengine walipiga magoti na kunywa kwa midomo. Gideoni akabaki na watu 300 waliochota maji na wengine wakarudishwa nyumbani.

8.6 Badala ya silaha, kila mtu alipewa mwenge uwakao ndani ya mtungi na tarumbeta. Walikuwa na imani kuu kwa kuenda vitani bila silaha.

8.7 Wamidiani walipiga kambi ndani ya bonde kubwa. Waisraeli kwa haraka na bila sauti walizunguka hilo bonde.



Wakapiga tarumbeta, wakavunja mitungi na kupiga kilele, "Upanga wa Bwana na wa Gideoni." Wamidiani waliogopa. Hawangeweza kutoka kambini kwa sababu walizungukwa na kwa ajili ya giza walianza kuuwana wenyewe. Hapa Waisraeli waliwashambulia.

8.8 Kwa hivyo jeshi ndogo la Israeli walishinda Wamidiani waliokuwa wengi na wa nguvu, bila kutumia silaha. Hakuna aliyekufa kwa hao watu 300. Ni kwa sababu waliamini Mungu. Mungu aliwabariki kwa miaka 40 kwa kukubali yeye awe mfalme wao.